

Ripoti yafichua wizi, ufujaji na utumiaji mbaya wa pesa hizo

# UPORAJI MIKUBWA WA CDF

Na JOY WANJA

**PESA za Ustawi wa Maeneo Bunge (CDF) zimeliwa vibaya tangu hazina hiyo ianzishwe miaka minane iliyopita, inasema ripoti iliyotolewa jana.**

Ripoti hiyo, ambayo ilitolewa jana na chama cha kitaifa cha kutetea walipaji kodi cha National Tax Payers Association (NTA) imefichua wizi na ufujaji wa pesa hizo.

Habari hizo zimetolewa huku hatima ya Hazina ya CDF ikiwa haijulikani vyema, hasa baada ya Waziri wa Fedha, Bw Uhuru Kenyatta, kusema huenda ikaondolewa.

Bw Kenyatta alisema hazina hiyo na ile ya maeneo ya wadi (LTF) zitaondolewa ili

maendeleo yafikie wananchi mashinani kuambatana na Katiba mpya.

Kulingana na ripoti hiyo, eneo la Ugenya ambalo ni



**ENDELEA UK 2**

# Uporaji wa CDF

**KUTOKA UK 1** la Waziri wa Ardhi, Bw James Orenge, ndiko pesa za CDF zimetumiwa vibaya zaidi miongoni mwa maeneo yaliyochunguzwa.

Eneo la pili kwa kutumia pesa vibaya ni Bumula, kwa Bw Bifwoli Wakoli na la tatu ni Kanduyi, linalowakilishwa na Bw Alfred Khang'ati. Maeneo haya mawili yamo mkoani Magharibi.

Ripoti hiyo inasema haku-na uwajibikaji kuhusu jinsi kamati za CDF katika maeneo hayo zinavyotumia pesa.

Inasema kati ya Sh182.2 milioni ambazo eneo la Ugenya lilipata kutoka 2003 hadi 2008, Sh5.1 milioni zimefujiwa katika miradi duni.

Pesa hizo ni sawa na asilimia 28 ya pesa zote ambazo eneo hilo limepata tangu CDF ianzishwe. Kati ya miradi 52 iliyoanzishwa Ugenya, 18 ilitekelezwa vyema na ikamilika ilhali mingine tisa ingali inaendelea.

Hata hivyo, mingine 15 ilitekelezwa vibaya sana na haijakamilika, ilhali mingine 10 haipo kabisa ingawa ilitengewa pesa.

Miradi iliyotengewa pesa na ingawa haipo ni ujenzi wa madarasa katika shule za msingi za Mbosie, Uriya Magoya, na Ywaya. Zilitengewa jumla ya Sh600,000.

Jumla ya Sh18.7 milioni zilifujwa katika eneo la Kan-

duyi kutokana na ufadhili wa miradi ambayo haijaonekana. Pesa hizo zilinuiwa kuchimba kisima cha Sango na kukarabati wa shule za msingi za Chemche na Chemuche miongoni mwa miradi mingine. Jumla ya Sh3.3 zilifujwa kupitia miradi duni katika Eneo Bunge la Starehe, Nairobi, linalowakilishwa na Askofu Margaret Wanjiru.

Sh5.6 milioni zilizotengewa Starehe pia hazikutumika kwa sababu miradi iliyokusudiwa ilicheleweshwa.

Katika Eneo Bunge la Makueni, jumla ya Sh1.6 milioni zilitumiwa vibaya katika miradi ambayo haikukamilika na mingine haipo.

Miradi miwili iliyotengewa pesa na haipo ni uwekaji mataa katika barabara ya Kirinyaga na ujenzi wa ukumbi wa jamii wa Pequinene uliokusudiwa kuwa mtaani Mathare. Ujenzi wa ukumbi huo ulitengewa Sh5.6 milioni.

Ripoti hiyo inasema hivi kuhusu Eneo Bunge la Kasarani, "Kwa mujibu wa barua ya halmashauri ya CDF, Sh500,000 zilipelekwa katika miradi mingine na Sh500,000 zilizosalia hazijulikani zilikio."

Asilimia tano ya pesa zilizotengewa Kasarani zilifujwa. Mbunge wa eneo hilo ni Bi Elizabeth Ongoro.